**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

Shule ya Sekondari Nandonde,
S.L.P.25,
Tandahimba-Mtwara
19/04/2024 .

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi**
**…………………………………………….................**
**S.L.P ………………………………………….................**
**…………………………………………….................**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO (FV-..............) KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA KUTWA NANDONDE HALMASHAURI YA WILAYA YA TANDAHIMBA MKOA MTWARA MWAKA 2024**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024 na atasoma **tahasusi ya** …………….........

Shule ya Sekondari Nandonde ipo umbali wa Kilometa 03 (03km) kutoka ofisi ya HALMASHAURI ya wilaya ya Tandahimba.Usafiri wa pikipiki kutoka stand kuu ya mabasi ya Tandahimba mjini unapatikana Nauli ni Shilingi 1,000/= tu na kwa bajaji SH.2,000/=
Shule iko nyuma ya ofisi za ujenzi jirani na shule ya msingi Nandonde.
Muhula wa Masomo unaanza tarehe **01/07/2024** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **01/07/2024** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **07/07/2024**

## 2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:-

### 2.1. Sare za Shule

**WAVULANA**

a) Mashati mawili meupe ya mikono mirefu na yenye mfuko usio kuwa na mfuniko na yawe marefu yanayoruhusu kuchomekewa.
b) Suruali mbili za KAKI (KAKI POLISI) yenye rinda **kitambaa kizito (ISIWE MODAL) na chini iwe Kuanzia inch 16**
c) Viatu vyeusi vya ngozi vyenye gidamu (kamba)
d) Soksi nyeusi jozi mbili
e) Suruali lazima ivaliwe na mkanda mweusi na siyo utambi
f) Sweta nzito rangi ya kahawia ( BROWN).
g) T- shirt ya shule rangi ya kijivu (zinapatikana shuleni)

Sare za Michezo iwe bukta nyeusi, t-shirt nyeusi (jezi nyeusi) na raba za michezo.

**NB:**Ni marufuku kuchanganya sare za michezo/kazi na zile sare za kuvaa wakati wa masomo.

**Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari counter book 10 za Quire 3
ii. **Ream (A4) ya Karatasi Mbili (2) kwa kila mwaka**;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha iambatishwe*);
iv. Dawa ya kufanyia usafi chooni lita 5
v. Nguo za ndani za kutosha;
vi. Ndoo ndogo (lita Kumi) Yenye mfuniko;
vii. Jembe 1, mifagio miwili (2) wa ndani na nje.

### 2.2. Michango mbalimbali

Nandonde sekondari ni Shule ya Kutwa;hivyo utalipia michango kama ifuatavyo**;**

| Na | AinayaMchango | Kiasi TSH |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 35,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **JumlaTSH.** | **50,000/=** |

Fedha hii ya michango **JUMLA TSH.50,000/=** ilipwe kupitia akaunti namba **71010004873** jina la akaunti ni **NANDONDE SECONDARY SCHOOL** iliyoko benki ya **NMB** na mwanafunzi aje na nakala ya risiti ya benki (bank pay in slip) shuleni ataikabidhi kwa mhasibu wa shule

**NB:Jina la mlipaji liandikwe jina la mwanafunzi na siyo jina la Mzazi/mlezi.**

## 3.Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu kwenye masomo
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya mipaka ya shule wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari;
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Shule ni ya kutwa hivyo mzazi atatakiwa kumpangia mwanae nyumba au chumba jirani na shule**
- **Mzazi atamgharamikia kijana wake pango na huduma muhimu kama vile chakula na matibabu**
- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule
vi. Kufuga ndevu;
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji wa sigara;
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xi. Kusababisha mimba;
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wakutoshiriki katika migomo, fujo na makosa yajinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wakaribu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.**Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.**

**TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBAZILIZOANDIKWA HAPO JUU.**

**HONGERA SANA**

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI NANDONDE**

……………………………………….

**MBONI I AHMAD**

**MKUU WA SHULE NANDONDE SEKONDARI**

**Mawasiliano**

**Mkuu wa Shule…0689811355**

**Makamu Mkuu wa Shule…0719039856**

**Mwalimu wa taaluma: 0768370698**

**Mwalimu wa** nidhamu **:0783511509**

**FOMU A**

**FOMU YA KUKUBALI MASHARTI**

**SEHEMU A: (IJAZWE NA MWANAFUNZI)**

Mimi .......................................................nimesoma na kuelewa kabisa masharti yote na sheria za shule na kuyakubali kwahiyo naipokea nafasi niliyopewa na serikali.

**Naahidi kuwa nitazingatia masharti na sheria zote za shule na nitakuwa mtiifu**.

Saini ya Mwanafunzi.............................................................

**SEHEMU B: (IJAZWE NA MZAZI/MLEZI**)

Mimi ........................................................................................................................ mzazi/mlezi wake nathibitisha kuwa mwanangu.......................................................................ameelewa maagizo yote na ninataka ifahamike kuwa dini ya Mwanangu ni...........................madhehebu ya ..................**.**

Wakati wa shule endapo nitahitajika na ikatokea kwamba sipo wafuatao wanaweza kuniwakilisha au kuja kumtembelea mwanafunzi.(**Andika majina kamili na namba zao za simu na ambatanisha na picha za passport zao kweye fomu hii.)**

| Na. | JINA | UHUSIANO NA MZAZI/MLEZI | NAMBA YA SIMU | PICHA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | |
| 2 | | | | |
| 3 | | | | |
| 4 | | | | |
| 5 | | | | |

Kama vile haitoshi nikiwa mzazi/mlezi ninaahidi kuhudhuria vikao vyote vya wazazi na walezi shuleni kwa kadri taarifa zitakavyokuwazikitolewa na uongozi wa shule kwa habari ya vikao vya wazazi.

Pia nakubaliana na sheria na kanuni ikiwemo kulipa michango na maeleke zomengine yatakayotolewa na shule.

…………………………………………………………….. ……………………………

**JINA LA MZAZI/MLEZI** **SAINI**

**NAMBA YA SIMU YA MZAZI ……… …………………TAREHE……………………**

**FORM B**

**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**TANDAHIMBA DISTRICT COUNCIL**

**NANDONDE SECONDARY SCHOOL, P.O.BOX 25, TANDAHIMBA**

**FORM FOR MEDICAL EXAMINATION**

**(To be completed by a medical Officer in respect of all form one/five entrants)**

Student`s full name…………………………………………………………………………………………

Age…………………………Sex…………………………………………………………

Blood count (Red and white)……………………………………………………………………

Stool examination………………………………………………………………………………….

Urine analysis…………………………………………………………………………………………..

Syphilis test………………………………………………………………………………………

TB test……………………………………………………………………………………..

Ears……………………………………… Eyes ………………………………………………

Chest………………………………………………………………………………………

Spleen…………………………………Abdomen………………………………………………….……

**ADDITIONAL INFORMATION**

e.g.physical defects or impairment(s), chronic infections or family diseases

…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………

I certify that the above named student is capable /is not capable to pursue studies.

Name…………………………………………………………………Designation……………………

Station………………………………………………………………Date…………………………………

**Note:Medical Officer** :

At a time of examination,please indicate the individual for any ailments you note.

**NB: Completed form should be sent to school with your acceptance form or brought as your report at school. No student will be enrolled without certificate of physical fitness.**

**FOMU C**

**I :HISTORIA YA MWANAFUNZI**

Jina la Mwanafunzi……………………………………………………………… jinsi……………

Tarehe ya kuzaliwa……………………Mtaa……………………………kata………………………

Jina la baba………………………………………Jina la mama …………………………………

Dini ya mwanafunzi…………………………………………

**II : MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MGOMO, FUJO,UTORO NA MAKOSA YA JINAI**

Mimi…………………………………………………………………sitashiriki katika aina yoyote ya mgomo, utoro wa muda mrefu kuanzia siku tano (05) nakuendelea na Kufanya fujo zikazohatarisha usalama wa shule au makosa yoyote ya jinai kama wizi, kupata/kumpa mtu au kutoa mimba, kupiga au kupigana. Na endapo itatokea nimeshiriki basi sheria zifuatwe na adhabu kali zitolewe dhidi yangu kulingana na makosa nitakayo kuwa nimeyatenda.

Natambua na kuthibitisha kuwa nitajielimisha kwa kadri ya uwezo wangu wote na kutumia nafasi hii niliyopewa kutimiza malengo yangu ya kupata elimu kama matarajio ya Serikali yalivyo na siyo vinginevyo.

JINA LA MWANAFUNZI……………………………………SAHIHI………………Tarehe……………

**III: UTHIBITISHO WA KIONGOZI WA ENEO- MTAA/KATA ANAPOISHI MWANAFUNZI**

**(Sehemu hii ijazwe na Kiongozi wa Eneo analoishi Mwanafunzi)**

NATHIBITISHA KUWA MWANAFUNZI………………………………………………………

NI MKAZI WA MTAA……………………KATIKA KATA YA…………………………………

JINA LA KIONGOZI WA ENEO…………………CHEO……………………MHURI

**ORODHA YA VITABU WANAVYOTAKIWA KUNUNUA WAZAZI/WALEZI**

Mwanafunzi anashauriwa kuwa na vitabu vya masomo yake yote (**GENERAL STUDIES, HISTORY LANGUAGE na KISWAHILI**) ambavyo vimeandikwa na "**TIE**"
Aidha kwa vitabu vya "**fasihi"** na "**Literature**" anashauriwa kuwa na vitabu muhimu vifuatavyo:-

**KISWAHILI**
- **Kimbunga**- H. Goro
- **Fungate ya Uhuru**- M.S. Khatibu
- **Chungu Tamu**- T. A. Mvungi
- **Vuta N'kuvute**-S.A.Shafi
- **Usiku Utakapokwisha**- M. Msokile
- **Mfadhili**- H. Tuwa
- **Morani**- E. Mbogo
- **Nguzo Mama**- P. Muhando
- **Kivuli Kinaishi**- S. Mohamedi
- **Kiswahili Sekondari**- Kidato cha V & VI Oxford
- **Kiswahili Sekondari**- Kidato cha Tano (TIE)
- **Kiswahili Sekondari**- Kidato cha Sita (TIE)

**ENGLISH LANGUAGE**
- Ashel, N. (2009) **Advanced Level English A Practical Approach**- DSM• Kadeghe Michael (2011) **The Real English Textbook for Advanced Level (Form Six)**-DSM
- Kadeghe Michael (2011) **The Real English Textbook for Advanced Level (Form Five)**-DSM
- **English Language for Secondary Schools, Language & Usage**- Form Five & Six Papers (TIE)
- **Advanced English Language Form Five & Six**- Oxford
- Ashel, N. (2011) **Advanced Level Literature,** The Essential Guide- GoodBook Publishers, DSM
- **Advanced Level Literature,** (2008) Nyambari Nyangwine Publishers, DSM
- Achebe, A. (1966) **A Man of the People**
- Ayi Kwei Armah (1968) **The Beautiful Ones Are Not Yet Born**
- Ibsen, H. (1982) **An Enemy of The People,** EA-DSM
- Imbuga, F.C (1976) **Betrayal in the City**
- Ngugi wa Mirii & Ngugi**IWillMarry**wa**When**Thiong'o**IWant,**EAEP-DSM(1982)
- **Selected Poems**, TIE
- Mloka, C. (2007) **The Wonderful Surgeon**

**HISTORY 1**

1.History 1 for secondary schools by TIE

2. History 1 by Salehe Yasini

3.History 1 by Bakari Madaya

**HISTORY 2**

1. History for secondary schools by TIE
2. History 2 by Salehe Yasini
3. History 2 by Madaya